TANGAZO LA SERIKALI NA. 454 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MABADILIKO YA MPAKA WA MSITU WA HIFADHI MKWENI HILLS YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Mabadiliko ya Mpaka wa Msitu wa Hifadhi Mkweni Hills ya Mwaka 2024.

Tangazo

Ts. Na. 7 la 1953

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Tangazo la Msitu wa Hifadhi Mkweni Hills linafanyiwa mabadiliko kusomeka na kuonekana kama lilivyochorwa katika Ramani iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

## JEDWALI

(*Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*


WILAYA ZA KAHAMA NA BUKOMBE

MSITU WA HIFADHI MKWENI HILLS

*Makadirio ya eneo:* Hekta 15770.00 au Kilometa za Mraba 157.70

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Msitu wa Hifadhi Mkweni Hills linalopatikana katika Wilaya za Kahama na Bukombe, mikoa ya Shinyanga na Geita mtawalia kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2840 ya mwaka 2012 (Skeli 1:25,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:




| | |
|---|---|
| Dodoma, | ANGELLAH JASMINE KAIRUKI |
| ___24 Mei, 2024 | *Waziri wa Maliasili na Utalii* |